

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZWA KWA MUDA WA KUJISAJILI KATIKA MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI

Ofisi ya Waziri Mkuu inapenda kuwashukuru Waajiri wote Tanzania Bara waliotekeleza agizo la Serikali la kujisajili katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) mpaka sasa. Agizo hili lilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu tarehe 27 Julai, 2017. Kutokana na mwitikio mkubwa wa Waajiri kujisajili na kuwepo kwa maombi mengi ya kuongeza muda wa kujisajili baada ya muda uliowekwa awali kumalizika tarehe 31 Agosti, 2017, Serikali imeridhia maombi hayo na kuongeza muda wa kutekeleza agizo lake hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2017.

Hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Waajiri ambao watakuwa bado hawajajisajili katika Mfuko kuanzia

tarehe 1 Oktoba, 2017.

**IMETOLEWA NA
MKURUGENZI MKUU
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
S.L.P. 79655, DAR ES SALAAM
Barua Pepe: info@wcf.go.tz; Tovuti: www.wcf.go.tz**